JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN

# MSLAC

# SHERIA BULLETIN

Toleo la 13



## Kampeni ijikite kutafuta suluhu na sio nani mshindi

— Mhe. Dkt. Doto M. Biteko —


***Bodi ya Uhariri***

**Mary Makondo**
KATIBU MKUU

**Lusajo Mwakabuku**
MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO CHA SERIKALI

William Mabusi
Hyasinta Kissima
Athman Msosole
Ibrahim Joseph
Neema Uiso


*Jarida Maalum*

# MSLAC ITUMIKE KUTAFUTA SULUHU NA SIO MSHINDI - BITEKO



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Mkoani Njombe,*

**Na Hyasinta Kissima**
**- WKS NJOMBE**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko amewataka watoa huduma za Msaada wa Kisheria kuitumia kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika kufanya utatuzi wa migogoro badala ya kutafuta mshindi miongoni mwa jamii.

Dkt. Biteko aliyasema hayo Mei 26, 2024 wakati wa uzinduzi wa kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campain) Mkoani Njombe iliyofanyika katika Halmashauri ya Mji ya Njombe.

Biteko amesema kuwa, ni vyema Wananchi kuacha misimamo iliyopitiliza wakati timu ya Mawakili itakapokuwa inawasikiliza na badala yake wasimamie kwenye ukweli.



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akisoma hotuba kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi.*

**"Maandiko yanasema ukijua kweli itakuweka huru nawe utakuwa huru kweli kweli na mawakili simamieni ukweli mtapokuwa mnasikiliza watu hawa watakaokuja kwenu,"**

Aliendelea kusema,"Migogoro iliyopo ya jamii miongoni mwenu iweze kuisha bila ya kusababisha madhara makubwa, ukiona mahali fulani mtu amenyanyua upanga akamuumiza mtu mwingine, ukiona mahali fulani mtu ameamua kumuua mtu mwingine ujue kuna shida. Ukiona mahali fulani mtu ameamua kumfanyia ukatili mtu mwingine au mahali fulani mtu ameamua kumnyanyasa mtu mwingine ni kwa sababu kuna mazingira ya kutokutambua wajibu wa kila mmoja miongozi mwa jamii." Alisema Dkt. Biteko.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliunda kamati ya tume ya haki jinai ambayo lengo lake ilikuwa ni kuboresha mfumo wa upatikanaji wa haki kwa umma.

"Tume ile ilikuja na mapendekezo iliona mambo mengi ndani ya jamii ambayo migogoro mingi ambayo ipo kwenye jamii, miongoni mwa migogoro hiyo migogoro ya ardhi, masuala ya mirathi, na utawala bora maana yake sisi viongozi tumekuwa sehemu ya migogoro hiyo," alisema Dk. Biteko.

Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Pindi Chana alisema tangu kuzinduliwa kwa kampeni ya msaada wa Kisheria ya Mama Samia jumla ya mikoa saba imefikiwa.

Dk. Chana aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Ruvuma, Shinyanga, Singida, Simiyu, Manyara, Dodoma na sasa mkoa wa Njombe.




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea tuzo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyokabidhiwa na Wizara ya Katiba na Sheria*

Alisema katika mikoa sita migogoro 5,16 imetatuliwa kati ya 4,942 na kufikia wananchi 4,15,000.

Aliwataka wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi ili kupata fursa ya msaada wa kisheria kupitia kampeni hiyo itakayofanyika kwa muda wa siku 10.



*Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo.*



*Mhe. Dkt. Doroth Gwajima Waziri - MJJWMM*



*Bi. Lulu Ngwanakilala, Mkurugenzi LSF.*

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo amesema kuwa kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Wanachi wenye matatizo mbalimbali ya Kisheria wamefikiwa na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria bure na kutatua changamoto katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua rasmi Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Mkoani Njombe, Mei 26, 2024.*




# KARIBU TUKUHUDUMIE!

Na Lusajo Mwakabuku

Ikiwa ni siku ya pili toka uzinduzi wa MSLAC ndani ya mkoa wa Njombe katika viwanja vya stendi ya zamani, viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa pamoja wameungana na wataalam kutoa huduma kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuongea na wananchi wanaopata huduma na kukagua utoaji wa huduma kwenye mabanda.

## HUDUMA ZINAZOTOLEWA

- Elimu ya kisheria,
- Msaada wa kuandaliwa nyaraka,
- Vyeti vya kuzaliwa na usajili,
- Utatuzi wa migogoro,
- Ukatili wa kijinsia,
- Masuala mbalimbali ya kisheria

## KWA NINI NI BURE?

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, imepewa jina hilo kutokana na maono ya Rais wetu juu ya upatikanaji Haki kwa wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili pale wanapopigania Haki zao hasa walio pembezoni, wanawake na watoto.

## TUNATEKELEZA!



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akimhudumia mwananchi.



Mhe. Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria akitoa huduma bandani.

## Mama Samia Legal Aid Campaign:

Kampeni hii inafanyika kwa miaka mitatu kuanzia mwezi Machi, 2023 hadi mwezi Februari, 2026 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kampeni imejikita katika kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi hususan katika masuala ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi, usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala, na masuala yahusuyo haki za binadamu kwa ujumla. Utekelezaji wa kampeni unafanyika kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, Wanazuoni na Wadau wa Maendeleo. Lengo kuu la Kampeni ni ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini.

# MSLAC yafika gereza la Njombe.



**Na Hyasinta Kissima**
- WKS DODOMA

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini amesema kuwa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika maeneo ya vizuizi ikiwemo Magereza imelenga kutimiza dhamira ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuona haki inatendeka kwa Watanzania wote na kwa wakati.

Mhe. Sagini ameyasema hayo Mei 27, 2024 wakati alipotembelea katika Gereza la Njombe akiwa ameambatana na Katibu Mkuu wa Wizara Bi. Mary Makondo, Mkurugenzi wa Taifa wa Mashatka Sylvester Mwakitalu, wataalamu na wadau wa Sheria ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Mkoani Njombe.

"Yapo maeneo mbalimbali ambayo Kampeni hii imelenga kuyafikia ikiwemo Magereza ili kukabiliana na mapungufu yanayoweza kuwa yamejitokeza katika usimamizi wa Sheria. Wafungwa na Mahabusu tulionao wanategemea washauriwe ipasavyo. Katika maeneo walipokwama na wengine mpaka wanahukumiwa msamaha wa Mhe. Rais unatoka lakini jamii haiwataki kuwapokea. Tunatengeneza mazingira gani ya usuluhishi lakini hata katika mazingira ya kudhaminiwa hata katika dhamana zilizo wazi Wananchi hawapo tayari kuwadhamini tunafanya nini ili wawe raia wazuri."Alisema Naibu Waziri Sagini.

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo amesema kuwa Wizara kupitia mradi wa e-justice itawezesha upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya mifumo ya kimtandao katika Mahakama, Magereza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya kurekebisha Sheria na wadau wengine kadri fedha zitakapokuwa zinapatikana.





# TATUENI KERO ZA KISHERIA

## ZINAZOWAKABILI WANANCHI – Dkt. Kazungu

**Na William Mabusi**
- WKS MAKETE

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu amewataka Wataalam wanaotekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) kutatua kero za kisheria wanazokabiliana nazo wananchi na zile watakazoshindwa kutatua kuziacha zimeandaliwa nyaraka kwenda ngazi za juu kwa ajili ya kutatuliwa.

Dkt. Kazungu ameyasema hayo Mei 27, 2024 alipotembelea Timu inayotekeleza Kampeni ya Mama Samia katika Halmashauri ya Makete ambayo ilikuwa ikifanya mkutano na wananchi wa Kijiji cha Mago Kata ya Lupalilo.

"Tatueni changamoto za kisheria wanazokabiliana nazo wananchi hawa na kero zitakazowashinda kutokana na muda hakikisheni mnawaandalia nyaraka za kisheria ili waende ngazi zingine," alisema. Dkt. Kazungu aliwashukuru wananchi waliojitokeza kwenye kampeni hiyo na kutumia wasaa huo kuwazawadia pesa akina mama waliofika kwenye mkutano wakiwa na watoto wadogo.

Kabla ya kuanza kutekeleza kampeni Wilayani humo timu hiyo iliripoti ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kuongea na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Makete Bw. William Makufwe ambaye amewataka watekelezaji wa kampeni hiyo kutumia lugha inayoeleweka, "tumieni lugha nyepesi wakati mnatekeleza kampeni hiyo muhimu ya kutoa uelewa wa sheria ili Wananchi wawaelewe, lakini pia niwaombe kuangalia uwezekano wa kubadili ratiba yenu kwa kuongeza idadi ya vijiji kwa kuzingatia kwamba wananchi wetu ni wachache na baadhi ya vijiji viko karibu karibu."

Akifafanua juu ya fidia ya maeneo ya miradi, Bw. Advent Tweve, Afisa Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Makete amesema pale ambapo mradi umeombwa au kuibuliwa na kijiji ni wajibu wa kijiji kutoa eneo la mradi bure isipokuwa pale ambapo Serikali imeleta mradi na kupelekea uhitaji wa eneo, Serikali huwajibika kutoa fidia.

**"Mnapoibua miradi nakuhitaji eneo la mwanakijiji mwenzenu hakikisheni mnamwelewesha umuhimu wa mradi huo ili atoe eneo bure kwa hiari yake, tena mhakikishe mmeandikishana ili kuepuka migogoro hapo baadaye." Alisema Bw. Tweve.**

# LUDEWA
## WAIPOKEA MSLAC
# KWA KISHINDO!

**Na Lusajo Mwakabuku & Athman Msosole**
- WKS LUDEWA

Uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Compain - MSLAC) Mkoa wa Njombe umeambatana na zoezi la utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwenye kata na vijiji katika Halmashauri zote sita za Mkoa wa Njombe ikiwemo Wilaya ya Ludewa.

Akiwapokea wataalam wanaounda timu ya msaada wa kisheria kutoka taasisi mbalimbali za serikali na binafsi, Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Bi. Victoria Mwanziva alisema Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia imefika wakati muafaka na wananchi wa Ludewa walikuwa wanaisubiri kwa hamu kutokana na migogoro mbalimbali inayohusu masuala ya kisheria inayowakumba wananchi wake.

"Sisi wana Ludewa tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa Kampeni hii ya Kitaifa, Wataalam wa Kisheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria wapo Ludewa na sisi Wilaya ya Ludewa tumeipokea kampeni hii kwa mikono miwili na kazi inaendelea wilayani hapa" Alisema DC Mwanziva.

Aidha mara baada ya timu kuwasili wilayani hapo, baada ya kujitambulisha katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, timu ya wataalam wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya Bi. Manziva walielekea katika kituo cha Radio kilichopo Ludewa mjini (Rafiki FM) na kuelezea kuhusu ujio wa Mama Samia Legal Aid Campaign wilayani humo kabla ya kuendelea kutoa Elimu mashuleni na mkutano wa Hadhara kwa lengo la kuelimisha jamii na kusikiliza changamoto mbalimbali za Kisheria na kuzipatia ufumbuzi.

"Ludewa tumeibeba hii kampeni na tunaenda bega kwa bega na team iliyopo hapa, tunawashukuru sana kwani kampeni hii itatoa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi pamoja na kufanya uwakilishi kwa wale wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili na mahakamani lakini pia kupitia kampeni hii, mabaraza ya usuluhishi ya kata, watendaji wa vijiji na kata watajengewa uwezo na hivyo kuimarisha upatikanaji wa haki". Aliongeza BI Mwanziva.


Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Bi. Victoria Mwanziva

# Achaneni na Misimamo Hasi – DC Makete



*Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Polisi Wilaya ya Makete Afande Nicholous Chilemile akitoa mada ya ukatili wa kijinsia kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Ihela Kata ya Tandala katika kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Mei 28, 2024.*

**Na William Mabusi**
- WKS MAKETE

Mkuu wa Wilaya ya Makete Bw. Juma Sweda amewaasa wananchi kuacha misimamo hasi na kukubali ushauri wanaopewa na Wataalamu wanaotekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia kwani misimamo mingine inaenda kinyume na sheria na hivyo kuendelea kuchangia migogoro katika jamii.

Mkuu huyo wa Wilaya ameyasema hayo Mei 28, 2024 kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Ihela na baadaye kwenye Kijiji cha Ikonda wakati alipotembelea timu inayotekeleza Kampeni hiyo katika Halmashauri ya Wiliaya ya Makete na leo kampeni hiyo ilikuwa inatekelezwa kwenye Kata ya Tandala.

"Unaweza kuwa na msimamo wako lakini kumbe msimamo huo ni kinyume na Sheria kitu ambacho kitapelekea uendelee kuishi kwenye mgogoro usioisha halafu kuendeleza uhasama na visasi kwenye jamii. Hivyo nawasihi wananchi mkubali kushauriwa na kubali kuachia misimamo isiyo na manufaa kwani kwa kufanya hivyo utaruhusu furaha na amani kuingia moyoni kwako." Alisema.

Mkuu huyo wa Wilaya aliendelea kuwasihi wananchi kueleza bila woga wala wasiwasi changamoto zozote za kifamilia, ardhi na shida zingine za kisheria ili wasaidiwe na wataalamu hao. Aidha, alisema wataalamu watawashauri viongozi wao pale tu watakapokuwa wameelewa vizuri changamoto za wananchi.



**"Unaweza kuwa na msimamo wako lakini kumbe msimamo huo ni kinyume na Sheria"**
DC Sweda

# MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN IMESAIDIA - DPP






**Na Lusajo Mwakabuku**
**& Hyasinta Kissima**
- WKS NJOMBE

Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP), Mhe. Sylvester Mwakitalu, amesema ujio wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Legal Aid, umeisaidia ofisi yake kuyabaini mashauri yaliyochukua muda mrefu bila kufikia muafaka na kuyafanyia kazi.

DPP amesema wataalam kutoka ofisi yake wamekuwa wakiambatana na wataalam wengine kutoka Tume ya Haki za Binadamu, Dawati la jinsia la Polisi, Wanasheria na watumishi wengine kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na kutembelea vituo vya vizuizi yakiwemo magereza na kuongea na uongozi lakini pia na wafungwa na mahabusu waliokuwepo katika vizuizi.

"Ofisi yangu imeshiriki kikamilifu toka mwanzo wa kampeni hii lengo likiwa ni kubaini changamoto za kisheria zikiwemo upatikanaji wa dhamana kwa wafungwa wanaostahili pamoja na namna kesi zao zinavyoendeshwa".

Aidha DPP Mwakitalu amesema kampeni hii imesaidia kubaini changamoto mbalimbali zilizoibuliwa na mahabusu pamoja na wafungwa ambao hupewa nafasi ya kuzungumza na kupelekea ofisi yake kuangalia namna bora zaidi za kukwamua changamoto hizo katika maeneo ya vizuizi.

# MSLAC YAWAFUTA MACHOZI WALIOSHINDWA GHARAMA ZA MAWAKILI



**Na Hyasinta Kissima**
**-** WKS NJOMBE

Wananchi wa Kijiji cha Nundu Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji Njombe wamepongeza ujio wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia kutokana na huduma hiyo kutolewa bila malipo, ambapo awali ilipelekea Wananchi kudhulumiwa haki zao kutokana na wengi kushindwa kumudu gharama za Mawakili.

Wakizungumza kwa wakati tofauti tofauti mara baada ya timu ya wataalamu wa msaada wa kisheria kufika Kijijini hapo kwa lengo la kutoa elimu, baadhi ya Wananchi wa kijiji cha Nundu wamesema kuwa, Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kujipambanua kwa kuendelea kuwajali Wananchi, kuwafuta machozi na kuhakikisha haki inatendeka kwa kila Mtanzania bila kujali kipato cha chake.

"Wakati mwingine katika kudai haki inaweza kufikia hatua unakua haujaridhika na haujui uende wapi.Unaweza kuwa umeingia kwenye mgogoro na mtu mwenye uwezo wa kuwa na Mawakili au taasisi ambayo wapo Wanasheria hivyo unafikia hatua unakosa msaada haki inapotea.Msaada wa Kisheria wa Mama Samia sisi walala hoi tunaona mwanga" Alisema Innocent Mlange mkazi wa Kijiji cha Nundu

Bernard Isdory ni mkazi wa Kijiji cha Nundu ambaye yeye aliambata na shemeji yake (mke wa mdogo wake) akilalamika kuhusu mdogo wake kumtelekeza mkewe na watoto wawili na kuwafukuza katika nyumba waliokuwa wamejenga na kuishi pamoja awali na kwenda kuishi katika Mkoa wa Ruvuma.

Bernard anasema kuwa mara baada ya kuonana na wataalamu waliofika kijijini hapo kupitia kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, imewajengea uwezo wa namna ya kuendelea na shauri hilo na matarajio yao ni kuona mgogoro huo unafikia muafaka na haki inatendeka.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia imeendelea kuwafikia Wananchi katika Kata na Vijiji mbalimbali vya Mkoa wa Njombe ambapo Wananchi mbalimbali wameendelea kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo.



# MSLAC itusaidie, kuna migogoro imetushinda – DC KISSA



**Na Hyasinta Kissima**
- WKS NJOMBE

Mkuu wa Wilaya ya Njombe Mhe. Kissa Kasongwa amesema kuwa kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika Wilaya ya Njombe ipo migogoro ya muda mrefu ambayo imekua ikijadiliwa na kuhamishiwa kwa Viongozi mbalimbali lakini ufumbuzi wa migogoro hiyo umekuwa haupatikani.

Mhe. Kissa aliyasema hayo Mei 29, 2024 wakati akiwasilisha salamu za Serikali katika Mkutano wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe uliofanyika katika ukumbi wa makao makuu ya Halmashauri yaliyopo Kijiji cha Kidegembye Kata ya Lupembe Wilayani Njombe.

"Tunaupongeza uongozi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye chini ya uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria waliamu kuja na ubunifu wa kuleta huduma za Kisheria za bure Mama Samia Legal Aid.Kuna mifupa huko imetushinda Waheshimiwa Madiwani. Zipo kesi za miaka mingi sana Wananchi wanahamisha malalamiko kwa Viongozi mbalimbali kila anapokuja Kiongozi mpya kesi zinaanza upya na muafaka haufikiwi. Mama Samia Legal Aid ipo Wilayani kwetu na leo hii tutaanza na mgogoro wa Lupembe Saccos ambao naamini huu mfupa hautatushinda."Alisema Kissa

Mheshimiwa Kissa amesema kuwa, mgogoro wa Lupembe Saccos ni kero ambayo inawaumiza Wananchi wengi na wengi wanaona wanapoteza haki yao kutokana na Wanachama wa Saccos hiyo kuwekeza mamilioni ya fedha kwa kipindi kirefu na kwa sasa wanapokwenda kuomba fedha zao Saccos hiyo haina fedha za kuwapatia wanachama wake.

Kwa upande wake Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria Candid Nasua amesema kuwa, Kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia timu ya Wataalamu wakiwemo Wanasheria na Mawakili ipo kwa ajili ya kuhakikisha kila mgogoro unasikilizwa na kupatiwa ufumbuzi ili haki iweze kutendeka kwa kila anayestahili.

Dhumuni la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kuwa kila Mwananchi mwenye nacho na asiyekuwa nacho mwenye uhitaji wa huduma za Kisheria anasaidiwa na anapata haki yake bila gharama yoyote.



# Matukio katika Picha



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko akiwasili katika viwanja vya stendi ya zamani na kupokewa na viongozi wa Mkoa na Wizara




Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akiteta jambo na Mkurugenzi wa Manunuzi Bwn. David Mwangosi



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akimnyanyua mtoto aliyeletwa na mzazi katika banda la RITA.




Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akimsikiliza mwananchi katika banda la Wizara ya Katiba na Sheria Stendi ya Zamani Njombe.



Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Bi. Victoria Mwanziva akiwa meza kuu na wataalam wa MSLAC waliofika Ludewa



Wanawake wa Njombe wakitoa zawadi kwa Mgeni Rasmi Siku ya Uzinduzi wa MSLAC Njombe.

